



Kudai Gharama zako za Usafiri ikiwa wewe ni Mtafuta Hifadhi

Ikiwa wewe ni Mtafuta Hifadhi, hata kama ombi lako halijakubaliwa, unaweza kudai gharama za usafiri kutoka huduma ya afya. Hii inamaanisha kuwa tutakurejeshea gharama za nauli ulizotumia kwenye mabasi, treni au mafuta ya kukufikisha au kutoka hospitalini.

Kijikaratasi hiki kinaeleza utahitaji kuwa na nini ili kudai gharama za usafiri.

Kwa habari zaidi au ili kudai gharama zako nenda kwenye Ofisi ya Uhasibu. Inapatikana katika kila hospitali. Uliza mfanyikazi yeyote jinsi ya kuipata au waonyeshe kijikaratasi hiki.

Ni madai gani ninaweza kutoa?

Mabasi, treni, vivuko n.k – Tafadhali tunza tiketi zako na kisha uzilete kwenye Ofisi ya Uhasibu.

Magari – Tunaweza kukupa malipo ya kiwango cha maili kwa safari ya kwenda na kutoka hospitalini.

Kusindikiza – Iwapo unahitaji kusindikizwa kwenye miadi yako, msindikizaji wako pia anaweza kudai gharama za usafiri (tafadhali hakikisha hii inaidhinishwa kabla ya kufanyika)

Usafiri wa bei nafuu ndiyo pekee unaweza kulipiwa. Hatutarejesha gharama za tekisi isipokuwa zimeridhiwa na daktari wako, kwa mfano kutokana na matatizo ya kutembea.

Ninahitaji kuleta nini?

Ili karani wa fedha alipe gharama zako, lazima ulete -

1. Kadi yako ya Usajili wa Maombi (ARC). Ikiwa bado hunayo, unapaswa kuleta barua yako ya utambulisho.



2. Barua yako ya miadi au Fomu ya Madai ya Gharama za Usafiri wa Wagonjwa.

3. Ikiwa madai yako ni ya mabasi, treni, vivuko n.k tafadhali leta tiketi zako.

Unapoenda Ofisi ya Uhasibu, unaweza kuwaonyesha upande mwingine wa kijikaratasi hiki, ambao unaeleza kile wanachohitaji kufanya ili kukurejeshea gharama zako za usafiri.



Information for Cashier's Office

This leaflet has been produced specifically for asylum seekers wishing to claim travel expenses.

Asylum seekers, including failed applicants, qualify for reimbursement of travel expenses.

They must produce an Application Registration Card (ARC) as proof of their entitlement which details their name, date of birth and nationality as well as their photograph and fingerprints.



If this has not yet been issued they must present a time limited, standard acknowledgement letter which can be used until they receive an ARC.

Note that only asylum seekers are eligible - this does not apply to other types of application such as those made under Human Rights legislation.

It is unlikely that an asylum seeker will have access to a bank account so reimbursements should be made in cash.